

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
TAASISI YENYE VIWANGO VYA ISO 900:2015



TAARIFA KWA UMMA

WITO WA KUSHIRIKI KATIKA TUZO ZA WSIS, PICHA BORA NA UWASILISHAJI WA MIRADI YA TEHAMA KWA MWAKA 2024

Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kwa kushirikiana na Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya Habari (WSIS) na waratibu wake, linawaalika wadau wote kuchangia katika uwasilishaji wa miradi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye kanzidata ya WSIS ili.. kushiriki tuzo za WSIS 2024. Miradi hii inabidi iwe yenye kulenga kuhamasisha teknolojia bora za habari na mawasiliano kulingana na mpango-kazi wa WSIS na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Maelezo zaidi kuhusu ukusanyaji wa taarifa za miradi na tuzo za WSIS yanapatikana kupitia: www.wsis.org/stocktaking na www.wsis.org/prizes.

Aidha, Shindano la Picha la WSIS, linalofanyika kila mwaka, limefunguliwa kwa washiriki wote. WSIS inawakaribisha washiriki kuwasilisha picha zinazoonesha jinsi TEHAMA inavyochangia katika kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Washindi watatu wa Shindano hili la Picha watapokea zawadi wakati wa Mkutano wa Jukwaa la hadhi ya juu la WSIS+20.

Kwa maelezo zaidi fuata: www.itu.int/net4/wsis/forum/2024/PhotoContest.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inawahimiza wadau wote, zikiwemo taasisi za Serikali, sekta binafsi, taasisi za kimataifa na kikanda, asasi za kiraia na wanataaluma, kuwasilisha miradi au mipango inayoshajihisha nguvu ya TEHAMA katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Hairuhusiwi taasisi moja kuwasilisha zaidi ya mradi mmoja kwa kila kipengele. Wadau wanahimizwa kusoma na kuzingatia kanuni za uwasilishaji wa mradi na vigezo vya ushiriki vinavyopatikana kwenye tovuti ya tuzo za WSIS. Wadau wote wa WSIS wanahimizwa kuwasilisha miradi ya TEHAMA ambayo wanaamini inakidhi vigezo vya kutambuliwa na kukuzwa, ikiwemo miradi iliyo na isiyo chini ya umiliki wao.

Orodha ya miradi iliyochaguliwa itatangazwa tarehe **15 Februari 2024**. Wadau wa WSIS watashiriki kuipigia kura tarehe **15 Machi 2024**.

Miradi Kumi na Nane (18) itakayoshinda itatangazwa pamoja na miradi mingine **72** katika sherehe ya tuzo za WSIS 2024 kwenye tukio la mkutano wa kilele wa WSIS+20 utakaofanyika tarehe 28 Mei 2024. Miradi iliyoshinda itaoneshwa kwenye machapisho ya WSIS katika kipengele cha Mafanikio, aidha maelezo ya shughuli zote za mradi na shughuli zake yatachapishwa katika Ripoti ya Miradi ya WSIS 2024.

Ukomo wa mawasilisho yote ni tarehe **31 Januari 2024**.

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
Mawasiliano Towers
20 Sam Nujoma Rd.,
S.L.P. 474
14414 DAR ES SALAAM